# Wildlife Photographer of the Year

## Kategoria za Mpiga Picha wa Mwaka wa Viumbe-mwitu

### Wanyama katika Mazingira yao

Kuleta hisia ya mazingira ya anga na hisia ya sehemu –ikiwa na makazi asili kama sehemu kuu ya picha - kuonyesha jinsi mnyama ni sehemu ya lazima ya mazingira yake.

### Picha za Wanyama

Za kuonyeshasifa pambanuzi za kiumbe mmoja au kundi mwandani la wanyama kwa njia ya kuchochea mawazo au kumbukumbu.

### Tabia: Amfibia na Watambaazi

Za kuonyesha tabia hai ambayo inaongeza ufahamu wetu juu ya asili ya spishi.

### Tabia: Ndege

Za kuonyesha tabia ya kukumbukwa, isiyo ya kawaida au yenye kuchochea hisia.

### Tabia: Wasouti wa mgongo

Za kuonyesha tabia ya kuvutisha fikra au ya kukumbukwa ya kaumu ya wanyama wadogo wasouti wa mgongo - wawe wa ardhini, hewani au majini.

### Tabia: Mamalia

Za kuonyesha tabia ya kukumbukwa, isiyo ya kawaida au yenye kuchochea hisia.

### Bahari:–Mtazamo kwa Mapana

Kuripoti juu ya ushawishi muhimu na umuhimu wa mazingira ya bahari kwetu sisi au kwa sayari. Picha zinaweza kuchukuliwa juu au chini ya maji. Zinapaswa kuwa na ujumbe - wa kiishara au halisi - wa bahari kama mabwawa ya mengi ya ajabu au bahari kama viendeshatabia nchi na hali ya hewa, au kama mifano ya jinsi binadamuwanavyotumia mbaya, linda au rejesha mazingira ya bahari.

### Mimea na Kuvu

Kuonyesha asili ya mmea au kuvu au kuonyesha umuhimu au kazi wake katika mazingira yake au njia zake za kuendelea kuishi.

### Sanaa ya Kiasili

Zinazofananisha uzuri mwepesi au sanaa changamani ya mazingira asilia. Picha zinaweza kuwa za rangi au nyeusi na nyeupe na ingawa zinaweza zisifanane na vigezo vya kategoria nyingine, lazima zibaki kuwa za kimazingira asilia.

### Ndani ya Maji

Za kuonyesha maisha ya majini, iwe mazingira ya baharini au maji baridi. Picha zinaweza kulenga tabia ya wanyama au kuonyesha wanyama au mimea kama sehemu ya mazingira ya majini.

### Viumbe-mwituvinavyoishi Sehemu WaishizoBinadamu

Kwa kulenga jinsi viumbe asilia vinavyomiliki au ishi pamoja kwenye mazingira yaliyo zaidi na wanadamu au kwa jiji, iwe ni kunasa maajabu ya maisha ya kila siku au yale yasiyotarajiwa au yasiyoonekana kwa kawaida.

### Mbuga Kinamasi:– Mtazamo kwa Mapana

Kueleza umuhimu wa mifumo ya ikologia ya maji baridi, kuanzia vilele vya milima na mboji za nyanda za juu, mito na maziwa hadi kwenye delta, mabonde ya mafuriko, maziwa ya tope na mikoko. Picha zinaweza kuwa na msukumo wa kuvutia kupitia athari au uzuri wake au kuonyesha simulizi ya mazingira au uhifadhi ambayo inaonyesha umuhimu wa mbuga kinamasi kwa mazingira asilia na / au watu.

### Uandishi wa Habari Kupitia Picha

Kuchunguza uhusiano kati ya wanadamu na ulimwengu wa asilia. Picha zinaweza kuwa za kuchochea, kuinua, kuchochea fikira au kufunulisha, na inapaswa kuonyesha jinsi mitazamo, maamuzi na matendo yetu yanavyoathiri ulimwengu asilia.

### Tuzo la Uandishi wa Habari Kupitia Simulizi kwa Picha

Zikisimulia hadithi ya nguvu, picha hizi sita hadi kumi zinapaswa kuwa na ubora wa kibinafsi na uthabiti wa pamoja kiusimulizi. Hadithi zinaweza kuwa za kuchochea, kuinua, kuchochea fikira au kufunulishana zinafaa kuonyesha jinsi mitazamo, maamuzi na matendo yetu yanavyoathiri ulimwengu asilia. Wasilisha hadithi zenyepicha hadi 10, ambazo baraza la waamuzi litachagua zisizozidi sita.

### Tuzo la Nyota ya Kesho (kati ya umri wa miaka 18 hadi 26)

Kuonyesha mtindo na dhamira ya kisanii, sampuli hiiya picha bora kabisa za mpiga picha (picha sita hadi kumi zinazohusu vitu au mitazamo tofauti) unapaswa kuonyesha upana wa ustadi na maono lakini wenye ubora thabiti kila mara.

### Tuzo la Jalada la Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu(umri wa miaka 27 na zaidi)

Kuonyesha sampuli ya kazi bora kabisa ya mpiga picha, picha hizi (sita hadi kumi) zinapaswa kuendana pamoja vizuri, iwe kupitia mtindo au mtazamo fulani au kulenga mada fulani, lakini hazihitaji kusimulia hadithi moja.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.

# Wildlife Photographer of the Year

## Masharti ya Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu wa Mwaka

**Tafadhali zingatia kuwa kuingia kokote katika Shindano la Mpiga Picha wa Viumbe-mwituwa Mwakapapo hapo kutakuwa chini ya Masharti haya. Kama ukiingia, wewe mshindani ("wewe") lazima usome na uwajibike na Masharti haya kwani yanatengeneza mkataba wa kisheria kati yako na Natural History Museum Trading Company Limited.**

## 1. KUHUSU SHINDANO

(1) Shindano la Mpiga Picha wa Viumbe-mwituwa Mwaka(“Shindano”) linamilikiwa na Natural History Museum Trading Company Limited ("sisi"). Sisi ni kampuni tanzu ya biashara ya bodi la kimashirika inayoitwa Trustees of the Natural History Museum(“Jumba la Kumbukumbu”). Jumba la Makumbushoni shirika la hisani lisilotozwa kodi [charitable organisation] lililosajiliwa chini ya sheria za Uingereza. Faida tunayoipata ni ya aina ya zawadi inayotolewa kwa Jumba la Kumbukumbu na inaweza kutumika kusaidia shughuli zake ikiwa ni pamoja na bila kikomo Mashindano zaidi na utafiti wa kisayansi. Mawasiliano yoyote nasi kuhusu SShindano la Watu Wazima au Shindano la Vijana (isipokuwa kama imeainishwa vinginevyo hapo chini) yanapaswa kupitia kwenye anwani ya barua pepe: **wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk**.

(2) Shindano linajumuisha Shindano la Watu Wazima lililowazi kwa wapiga picha wenye umri wa miaka 18 na zaidi, na Shindano la Vijana lililowazi kwa wapiga picha wenye umri wa miaka 17 na chini.

(3) Kutangaza Shindano, picha zilizotuzwa Tuzo na Baraza la Waamuzi zinaweza kuonyeshwa katika:

- (i) maonyesho kwenye Jumba la Makumbusho ya Historia ya Asili (Natural History Museum) London (“Maonyesho ya WPY” - “the WPY Exhibition”);
- (ii) matoleo yafuatayo ya Maonyesho ya WPY yanayoendeshwa na wenye leseni katika nchi yoyote ("Ziara ya Maonyesho") na
- (iii) maonyesho yanayoendeshwa na sisi Jumba la Kumbukumbu au waliopewa leseni kwenye eneo lolote ambalo linaonyesha picha za Mashindano ya Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu wa Mwaka ("Maonyesho Yanayohusiana").

(4) Katika Masharti haya, Maonyesho ya WPY, Ziara ya Maonyesho na Maonyesho Yanayohusiana kwa pamoja yatajulikana kama "Maonyesho". Fungu la 8 hapa chini linaelezea haki maalum za leseni kuhusu utumiaji wa picha zilizopewa Tuzo.

(5) Shindano na maonyesho yatokanayo na hilo kwenye Jumba la Makumbusho la Historia ya Asili London yatokanayo ya mshindi au uwasilisho unaopendekezwa sana vinaweza kufadhiliwa na shirika ambalo litachaguliwa na sisi kwa hiari yetu pekee, ("Wa/Mfadhili Rasmi"). Kwa nyongeza, onesho la Ziara ya Maonesho kwa aliye na Leseni linaweza kufadhiliwa na Mfadhili (Wafadhili) tofauti kwa muda wa Onesho hilo la Ziara kama likitajwa na Mwenye Leseni ya Onesho la Ziara husika na kuidhinishwa na NHM kabla (“Mfadhili (Wafadhili) wa Ziara ya Onesho”).

## 2. KUINGIA KWENYE SHINDANO

(1) Uwasilisho kwenye shindano lazima uweumepokelewa ifikapo saa 11.30 asubuhi majira ya GMT, mnamo Alhamisi tarehe 05 Desemba 2024 (‘tarehe ya mwisho’).

(2) Shindano la Watu Wazima ni wazi kwa mtu yoyote aliyetimiza umri wa miaka 18 au zaidi Alhamisi mnamo tarehe 05 Desemba 2024, kasoro:

- (i) watu (na wenzi wao na familia) wanaohusika katika uandaaji au uamuzi wake; au
- (ii) waajiriwa wa Kampuni ya Natural History Museum Trading Company Limited, au Trustees of the Natural History Museum au ikiwa wanafahamika wakati wa kipindi cha kuingia halafu Wa/Mfadhili Rasmi.

(3) Kwa kuingia kwenye Shindano la Watu Wazima, unakubali:

- (i) kutii Masharti na kuhakikisha kuwa uwasilisho wakounaendana na Masharti;
- (ii) kuwa na viwango vya juu kabisa katika masuala yote yanayohusiana na Shindano; na
- (iii) kwamba utawajibika kwetu, na kwa Jumba la Makumbusho kwa uharibifu wowote au hasara yoyoteitakayotokea kwa mashirika hayo kwa sababu ya ukiukaji wako wa Masharti.

(4) Maingizo yote ni lazima yawe ni ya wanyama mwitu wasiokamatika, mimea, uyoga, mandhari na makazi, kasoro yale yaliyoainishwa katika sehemu ya 4.2 (iii).

(5) Maingizo yote ni lazima yawe matokeo ya mchakato wa upigaji picha kwa kutumia kamera.

(6) Hauruhusiwi kuwasilisha picha ambazo:

- (i) zinaonyesha mifugo, wanyama vipenzi, na/au mimea ya kupanda na fangasi;
- (ii) zinakiuka majukumu yoyote ya kimaadili yaliyotolewa hapa chini katika Sehemu ya 4 au mahitaji ya Sifa za Picha yaliyopangwa hapa chini katika Sehemu ya 5.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.

# Wildlife Photographer of the Year

(7) Uwasilisho katika shindano wowote utakaokutwa haufuati Masharti katika hatua yoyote ya Shindano la Watu Wazima unaweza ukafutwa. Hakuna marejesho au posho zozote zitakazolewa iwapo uwasilisho utafutwa na tuzo zozote ambazo hazijapokelewa zitabatilishwa na  ni lazima urudishe zawadi yoyote ya pesa na gharama ambazo umepokea ndani ya siku 14. Pindi ambapo ingizo limebatilishwa, tuna haki ya kuthibitisha kuwa ingizo lilibatilishwa kwa mujibu wa malalamiko yoyote.. Ikiwa ukiukaji umetokea, lakini unagunduliwa baada ya tuzo, basi tunaweza kuondoa uwasilisho kwenye Maonyesho na / au shughuli zinazohusiana zozote na kuhitaji kurudishiwa au kurejeshwa kwa tuzo yoyote iliyopokelewa tayari. Uamuzi wetu wowote unaohusiana na Shindano ni wa mwisho na wa mujibu. Hakuna mijadala itakayozingatiwa na hatutaingia katika mawasiliano baada ya hapo kuhusu maamuzi kama hayo.

(8) Pamoja na kwamba taarifa katika Masharti haya ni sahihi, sisi, kwa hiari yetu tu lakini tukiwa tunatatenda kwa busara, tunahifadhi haki bila kutoa taarifa kabla ya:

- (i) Kurekebisha Masharti bila marejesho;
- (ii) Kubadilisha tuzo kwa mujibu wa kifungu cha 6 (8);
- (iii) amua ikama sherehe yoyote ya tuzo ya Shindano itakuwa hafla au itafanyika kupitia mtandaoni tu;
- (iv) samehe ukiukaji wa Sheria bila kurejesha;
- (v) kufutaShindano na kusitisha mikataba na leseni zilizoundwa na Masharti hayakwa kuzingatia kurudishiwa ada ya kuingia kwenye shindano.

(9) Tuna haki zote za kubatilisha picha yako ikiwa mwenendo wako ni kinyume na ari au dhumuni la Shindano au Onesho.

## 3. SHINDANO LA WATUWAZIMA – KUWASILISHA

(1) Uwasilishaji lazima ufanyike kupitia www.wildlifephotographerofyeyear.com kabla ya saa 11.30 asubuhi majira ya GMT Alhamisi mnamo tarehe 05 Desemba 2024.

(2) Ada ya uwasilishaji ya mara moja tu na ambayo haitarudishwa ya £30.00 inahitajika kutoka kwa kila mshindani inaweza kulipwa hadi saa 11.29 za asubuhi, majira ya GMT mnamo Alhamisi 28 Novemba 2024. Kuanzia saa 11.30asubuhi majira ya GMT mnamo Alhamisi tarehe 28 Novemba ada ya mara moja tu na ambayo haitarudishwa ya uwasilishaji itakuwa £35.00 na inahitajika kutoka kwa kila mshindani.

(3) Ada ya ushiriki imeondolewa kwa washiriki wenye umri wa miaka 18 – 26 kufikia 05 Desemba 2024.

(4) Ili kuwezesha waombaji anuwai, ambao wanaishi katika nchi zozote zifuatazo hawatabidi kulipa ada ya uwasilishaji kama wanaweza kutoa ushahidi wakiombwa kufanya hivyo: Algeria, Angola, Antigua and Barbuda, Argentina, Aruba, Bahamas, Barbados, Belize, Benin, Bolivia, Botswana, Brazil, British Virgin Islands, Brunei, Burkina Faso, Burundi, Cabo Verde, Cambodia, Cameroon, Cayman Islands, Jamuhuri ya Afrika ya Kati, Chad, Chile, Colombia, Comoros, Jamuhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Congo, Costa Rica, Côte d'Ivoire, Cuba, Curaçao, Djibouti, Dominica, Dominican Republic, East Timor, Ecuador, Misri, El Salvador, Equatorial Guinea, Eritrea, Eswatini, Ethiopia, Gabon, Gambia, Ghana, Grenada, Guatemala, Guinea, Guinea-Bissau, Guyana, Haiti, Honduras, Indonesia, Jamaica, Kenya, Laos, Lesotho, Liberia, Libya, Madagascar, Malawi, Malaysia, Mali, Mauritania, Mauritius, Mexico, Morocco, Msumbiji, Myanmar, Namibia, Nicaragua, Niger, Nigeria, Panama, Paraguay, Peru, Philippines, Puerto Rico, Rwanda, São Tomé and Principe, Senegal, Seychelles, Sierra Leone, Singapore , Sint Maarten, Somalia, Afrika Kusini, Sudani ya Kusini, St. Kitts and Nevis, St. Lucia, St. Martin, St. Vincent and the Grenadines, Sudan, Suriname, Tanzania, Thailand, Togo, Trinidad and Tobago, Tunisia, Turks and Caicos Islands, Uganda, Uruguay, Venezuela, Vietnam, Virgin Islands (U.S.), Zambia, Zimbabwe.

(5) Shindano la Watu Wazima lina kategoria zifuatazo:

- (i) Wanyama katika Mazingira yao;
- (ii) Picha za Wanyama;
- (iii) Tabia: Amfibia na Watambaazi;
- (iv) Tabia: Ndege;
- (v) Tabia: Wasouti wa mgongo;
- (vi) Tabia: Mamalia;
- (vii) Mimea na Kuvu;
- (viii) Ndani ya Maji;
- (ix) Viumbe-mwituvinavyoishi Sehemu Waishizo Binadamu;
- (x) Sanaa ya Kiasili;
- (xi) Bahari: Mtazamo kwa Mapana;
- (xii) Mbuga Kinamasi: Mtazamo kwa Mapana;
- (xiii) Uandishi wa Habari Kupitia Picha;

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@
nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London. 

(xiv) Tuzo la Uandishi wa Habari Kupitia Simulizi kwa Picha;
(xv) Tuzo la Nyota ya Kesho (kati ya umri wa miaka 18 hadi 26); na
(xvi) Tuzo la Jalada la Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu (umri wa miaka 27 na zaidi).

(6) Unaweza kuwasilisha picha zisizozidi ishirini na tano (25) kwa ujumla bila kujali idadi ya kategoriahapo juu unazowasilishia. Hii ni pamoja na:
   (i) kati ya picha sita (6) na kumi (10) kwa Tuzo la Uandishi wa Habari Kupitia Simulizi kwa Picha kwa kila hadithi. Unaweza kuwasilisha hadi hadithi mbili (2) tu katika kategoria hii. picha zisizo zidi sita (6) zitachaguliwa na Baraza la Waamuzi.
   (ii) kati ya picha sita (6) na kumi (10) kwa Tuzo la Nyota ya Kesho ambazo picha zisizozidi sita (6) zitachaguliwa na Baraza la Waamuzi. Unaweza kuwasilisha jalada moja (1) tu kwa kategoria hii; na
   (iii) kati ya picha sita (6) na kumi (10) kwa Tuzo la Jalada la Mpiga Picha wa Viumbe-mwituambazo picha zisizozidi sita (6) zitachaguliwa na Baraza la Waamuzi. Unaweza kuwasilisha jalada moja (1) tu kwa kategoria hii.

## 4. MASHARTI YA UADILIFU

(1) Ukiukaji wowote wa Masharti ya Uadilifu hapa chini utakuwa ni ukiukaji wa Masharti

(2) Picha zako lazima ziwe zinataarifia juu ya ulimwengu asilia kwa njia ambayo ni ya ubunifu na ya uaminifu na ya kimaadili:
   (i) uwasilisho usiwe wa kidanganyifu kwa mtazamaji au kujaribu kujificha na/au
   (ii) kupotoshaukweli wa ulimwengu asilia;
   (iii) taarifa za manukuuzinazotolewa lazima ziwe kamili, za kweli na sahihi; napicha hazipaswi kuonyesha wanyama waliokamatwa, fungwa, tawaliwa kwa hila, sanamu za wanyama, ngozi ya wanyama nzima zilizojazwa vitu kurudisha ufanano wa mnyama hai na/au mnyama mwingine yoyote anayenyonywa kwa faida. Isipokuwa, wakati wakutolea taarifa suala maalum juu ya namna wanyama wanavyofanyiwa na mtu fulani, katika hali ambako lazima uelezee kwa dhairi kwamba mnyama alikuwa amekamatwa, amefungwa, amezuiliwa, ni sanamu au ngozi ya mnyama iliyojazwa vitu kuifanya ionekane ni mnyama hai.

(3) Haupaswi kufanya kitu chochote kuumiza au kufadhaisha mnyama au kuharibu makazi yake katika kujaribu kupata picha. Hii ni pamoja na kupita juu ya mnyama kwa kuruka angani na ndege (au kijindegemvumo) kwa chini sana au kwa kelele juu ya mnyama na picha za kwenye viota kwa kutumia lensi zenye pembe pana ijapokuwa lensi za picha za simu zinaruhusiwa. Ustawi wa mnyama lazima uwe na kipaumbele daima.

(4) Unawajibika kuhakikisha utekelezaji kamili wa sheria yoyote inayotumika kitaifa au kimataifa (pamoja na zinazohusiana na za vijindegemvumo) na kupata vibali vyovyote vinavyohusika (ambavyo, ikiwa ni picha za wanadamu, itajumuisha idhini ya mhusika) na ambavyo lazima tuweze kuvionakama tukiviomba.

(5) Kuweka chambo cha moja kwa moja hairuhusiwi, wala njia yoyote ya chambo ambayo inaweza kumweka mnyama hatarini au kuathiri vibaya tabia yake, ama moja kwa moja au kwa kutojali kuwa matendo yanajengea mazoea mnyama. Njia nyingine zozote za kuvutia, ikiwa pamoja na mbegu kwa ndege au kwa harufu, lazima zitolewe taarifa katika manukuu kwa ajili ya kupitiwa na baraza la waamuzi na sisi. Jopo la majaji litazipa kipaumbele picha zisizo na chambo.

(6) Ikiwa tunashuku kwambawasilisho limepatikana kwamatendo ya kikatili au yasiyo ya kimaadili, ikiwemo pamoja na matumizi ya chambo ya moja kwa moja au ya kutojali au kwa njia yoyote kukiuka Masharti haya, uwasilisho utafutwa na tunahifadhi haki ya kutaarifu kwa mamlaka husika juu yako.

## 5. SIFA ZA PICHA

(1) Picha ni lazima ziwe zilipigwa ndani ya miaka mitano iliyopita. Tarehe ya kupiga ni lazima iwe baada ya Oktoba 2019 na itolewe ushahidi ukiombwa.

(2) Jopo la majaji litakuwa likiangalia picha mpya, hivyo tunawaomba sana msiweke picha ambazo tayari zimetuzwa katika mashindano mengine sawia ya kimataifa (yaani mshindi, mshindi wa pili, pendwa, iliyotajwa kwa heshima n.k.). Jopo la majaji litapendelea sana picha ambazo bado hazijatuzwa tayari katika mashindano mengine.

(3) Uwasilishaji wako lazima upakiwe katika muundo wa JPEG lakini wasilisho la asili halihitaji kuwa limepigwa kwa kutumia kamera ya dijitali. Tambazo za ubora wa hali ya juu za angavu au za negativu za picha pia zinakubalika.

(4) Faili za kidijitalii lazima ziwasilishwe kama JPEG,zilizohifadhiwa katika mipangilio ya ubora wa hali ya juu wa angalau 8 katika Photoshop, Adobe RGB (1998), na kwa pikseli 1920 kwa upande urefu mrefu zaidi kwa kategoria zote. Jopo la majaji halitozizingatia picha ambazo zina mipaka, taswira fifi au saini.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.

(5) Ikiwa picha yako itawekwa kwenye orodha teule la muisho utahitajikutoa yafuatayo:

(i) Faili RAW(kwa mfano .ARW, .CR2/3, .NEF, .ORF, .PEF n.k.), au JPEG asilia ambazo hazijaguswa (na anuwai ya faili za "kabla" na "baada" za JPEG ambazo hazijaguswa); na angavu au negativu asilia, zitahitajika kwa uthibitishaji. Faili za DNG zinaruhusiwa tu ikiwa ndio muundo wa RAW asilia wa kamera;

(ii) Faili za mwonekano wa juu (ikiwezekana TIFF) zinazohitajika kwa uchapishaji zinapaswa kuwa 8-bit, Adobe RGB (1998) kwa mwonekano mzima, na zilingane na rangi na upunguzaji wa JPEG uliowasilishwa katika shindano. Tafadhali usiongeze ukubwa. Faili zisizidizidi 500MB.

(6) Uwasilisho wowote ambao hauwezi kuthibitishwa au sio waubora unaokubalika utafutwa. Tunahifadhi haki ya kukuomba uwasilishe anuwai ya faili za "kabla" na "baada" za picha yoyote ambayo inahitaji uthibitishaji zaidi.

(7) Tofauti na yale yaliyopangwa katika sehemu ya 5(8) hapa chini, marekebisho ya kidijitali ikiwa ni pamoja na rangi/toni na ulinganuzi, kuchoma, kukwepa, kukata, kunoa, kupunguza kelele, kazi ndogo ya kusafisha (kwa mfano uondoaji wa vumbi la kihisio au mikwaruzo kwenye angavu / tambazo, kuondolewa kwa upotovu utokanao na rangi kutolengeka vizuri, kupotosha lensi na kupunguza mng'ao wa picha pembezoni ukilinganisha na kati), HDR, panorama zilizounganishwa, na "uunganishaji"- kuunganisha picha na kuchanganya kwa lengo anuwai, kuchanganya mfichuo, kupunguza kelele, au kurefusha mfichuo ikiwa ilipigwa kwenye eneo hilo hilo kwenye karibia muda huo huo kama mfululizo endelevu au ndani ya kategoria ya Usanii Asilia kama tu mifichuo kadhaa katika kamera vinaruhusiwa ilimradivinazingatia kanuni za Shindanojuu ya uthabiti yaani hayamdanganyi mtazamaji au hayawakilishi visivyo ukweli wa ulimwengu asilia au kile ambacho kilinaswa na kamera hapo mwanzo.

(8) Ili kuepusha wasiwasi, marekebisho yafuatayo ya kidijitali hayaruhusiwi: kuongeza, kuhamisha au kuondoa vitu, wanyama au sehemu za wanyama, mimea, watu na kadhalika; kuondoa uchafu, mwangazio, utenganishonyuma, viputo, uchafu na vingine kama hivyo; picha zilizochanganywa kuwa moja, uchoraji mandharimbele/ uchoraji mandharinyuma au picha zilizozalishwa kwa akili bandia yaani AI. Kama njia yoyote ya baada ya kuchakata ikiongeza maudhui mapya ya picha kwenye picha kupitia kanuni za akili bandia yaani AI au kwa uingiliaji alisi, picha itakayotokea itakuwa imekiuka kanuni hizi.

(9) Taarifa za manukuu lazima ziwe kamili, za kweli na sahihi na zijumuishe maelezo juu ya nini kinatokea katika picha, kwanini picha hiyo ina maana, mwenendo ulioonwa; chanzo cha hadithi; eneo hasa (m.f. majira ya nukta ya GPS), mwaka ambao picha ilipigwa; kama chambo kilitumiwa, na kama ni hivyo, cha asili gani (angalia kifungu cha 4.5); na kama spishi hiyo ina umuhimu wa kisayansi. Wapiga picha wanahimizwa kuweka manukuu kwa ufupi-upeo lakini yenye taarifa za kina kwa herufi 2500.

(10) Haupaswi kuingiza jina lako kwenye manukuu au kwenye picha yenyewe. Hupaswi kujumuisha jina lako katika data ya faili lolote yaani mmiliki, hakimiliki au sehemu za watayarishi.

## 6. UAMUZI, TUZO NA ZAWADI

(1) Jopo la wataalam linalojumuisha mwenyekiti na majaji ('Baraza la Waamuzi"') litateuliwa na sisi ili kuchagua na kuzipa tuzo takriban wasilisho mia moja (100) kutoka kwenye Mashindano ya Watu Wazima na Vijana kwa ujumla.

(2) Baraza la Waamuzi litazingatia picha hizo kulingana na vigezo vya uchaguzi vinavyojumuisha uasilia, simulizi na desturi zakimaadili. Baraza la Waamuzi litapendelea picha ambazo hazijapewa tuzo katika mashindano mengine sawia ya kimataifa (ikimaanisha mshindi, mshindi wa pili, anayepongezwa, pongezi ya heshima n.k.) Baraza la Waamuzi itawekwa litatolewa kwenye tovuti ya Shindano **hapa**.

(3) Wakati wa maamuzi na kwa idhini yetu dhairi, Baraza la Waamuzi linahifadhi haki ya:

(i) kuhamisha wasilisho kutoka kategoria moja hadi nyingine pale inahusu na kufaa;

(ii) kutotoa tuzo katika kategoria fulani kwa njia iliyoelezewa katika kifungu cha 6 (4) hapa chini; au

(iii) kuondoa kategoria nzima yote.

(4) Kutoka kwenye mawasilisho yaliyochaguliwa na Baraza la Waamuzi kutoka kwenyeShindano la Watu Wazima, tuzo zifuatazo zitatolewa ("Tuzo"):

(i) Kategoria ya Lililopongezwa Sana;

(ii) Kategoria ya Mshindi; na

(iii) Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu wa Mwaka.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

# Wildlife Photographer of the Year

(5) Washindi wa Kategoria tu ndio watazingatiwa na Baraza la Waamuzikwa tuzo yaMpiga Picha wa Viumbe-mwitu wa Mwaka. Baraza la Waamuzilinahifadhi haki ya pia kujumuisha kwa ajili ya kuizingatiwa picha moja (1) waliyochaguaya Mshindi wa Kategoria ya kila mojawapo ya kategoria nyingi zifuatazo za picha:

(i) Tuzo la Uandishi wa Habari Kupitia Simulizi kwa Picha;

(ii) Tuzo la Nyota ya Kesho (kati ya umri wa miaka 18 hadi 26); na

(iii) Tuzo la Jalada la Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu (umri wa miaka 27 na zaidi).

(6) Tunataka kuhimiza na kutoa tuzo kwa picha ya mnyama mwitu ambayo inahamasisha matumaini na matendo chanya kwa ajili ya ulimwengu asilia. Baraza la Waamuzi linaweza likatoa Tuzo Maalum – Tuzo ya Athari - ndani ya picha 100 zilizoshinda katika kategoria yoyote, kutambua mafanikio ya uhifadhi, hadithi ya matumaini na/au mabadiliko chanya. Hata hivyo, mshindi wa tuzo hatozingatiwa kwa ajili ya taji la Mpiga picha wa Mwituni wa Mwaka, isipokuwa kama ni mshindi wa kundi.

(7) Picha nyingine ishirini na tano (25) kutoka Awamuya Mwisho ya Shindano la Watu Wazima na Shindano la Vijana zitachaguliwa na Baraza la Waamuzi na sisi na kuweza kupatikana kwa umma kwa miezi mitatu (3) kwa ajili ya kupigiwa kura mtandaoni. Mawasilisho hayayatafanyiwa matangazohasa kupitia mitandao ya kijamii na kupitia wabia wetu wowote wa magazeti au wa kibiashara. Uwasilisho utakaopigiwa kura nyingi zaidi utapokea Tuzo Maalum la Chaguo la Watu, na mawasilisho manne (4) yafuatayo kwa kupendwa sana yatapongezwa sana. Pamoja na hayo, mshindi wa Tuzo Maalum la Chaguo la Watu hatazingatiwa kwa Mpiga Picha wa Viumbe-mwitu wa Mwaka.

(8) Ukifanikiwa, utaarifiwa kwa usiri sana. Hili ni sharti la kuwasilisha katika Tuzo lolote na zawadi yoyote kwamba haufichui maelezo juu ya mawasilisho yaliyo kwenye orodha teule au yanayoshinda kwa mtu yeyote mwingine.

(9) Orodha ya zawadi inapatikana kwenye **tovuti**. Haiwezi kuhamishwa. Tunahifadhi haki, kwa hiari yetu, kubadilisha zawadi yoyote iliyoorodheshwa, yote au sehemu yake, na zawadi mbadala yenye thamani ya kifedhaau ya utangazaji sawa (lakini hautakuwa na haki yoyote ya kudai hili). Tafadhali zingatia kwamba zawadi lazima zidaiwe ndani ya mwaka mmoja wa kutaarifiwa juu ya mafanikio, au ambapo ni zawadi yenye tarehe maalum ya tukio iliyopangwa basi hadi mwezi mmoja (1) kabla ya tarehe hiyo ya tukio, au kwa kila hali itafutwa (pamoja na haki yoyote ya kupokea zawadi au utangazaji wowote mbadala).

## 7. UTANGAZAJI

(1) Unakubali kwamba, ikiwa kiingilio chako kitachaguliwa na Baraza la Waamuzi, au na umma kama sehemu ya Tuzo Maalum ya Chaguo la Watu, utashiriki kwa kiwango kinachofaa cha utangazaji unaohusiana na ukubali matumizi ya jina lako na sura yako kwa madhumuni ya kutangaza, kukuza na utangazaji wa Mashindano na / au Maonyesho ya WPY na / au Maonyesho yoyote yanayohusiana bila fidia ya ziada.

## 8. HAKI YA MALI YA AKILI NA LESENI

(1) Picha yoyote unayowasilisha kwa shindano lazima iwe:

(i) Picha yako ya asili iliyopigwa kwenye kamera; au

(ii) Picha asilia iliyopigwa kwenye kamera na mpiga picha lakini iliyowasilishwa na wewe kwa niaba ya mpiga picha, katika hali hiyo lazima utujulishe jina la mpiga picha na ukiombwa na sisi lazima utoe uthibitisho wa kimaandishi kutoka kwa mpiga picha kuwa unaidhini ya kutenda kwa niaba yake na kwamba yeye mwenyeweanakubali kabisa na kuwajibika na Masharti haya zenyewe.

(2) Lazima uwe mmiliki pekee wa hakimiliki ya picha katika (ma)wasilisho au uwe umepata idhini ya kimaandishi ya mmiliki wa hakimiliki au wamiliki wowote wa pamoja wa hakimiliki kuwasilisha uwasilisho kwenye Shindano. Nakala ya idhini yoyote kama hiyo ya kimaandishi lazima ifikishwe kwetu pale utakap thibitishiwa kwamba picha yako imewekwa kwenye orodha teule kwa ajili ya Tuzo.

(3) Umiliki wa hakimiliki katika uwasilisho wowote uliowasilishwa kwenyeShindano utabaki na wa/mmiliki wa hakimiliki.

(4) Kwa kuzingatia nafasi ya kushinda Tuzo kwa picha unayowasilisha kwa Mashindano, unatupatia sisi na Makumbusho haki ya kuzaa tena, kutangaza na kuonyesha picha hizo kwa njia yoyote (pamoja na lakini sio kwa nakala halisi. , nakala za elektroniki na kwenye media ya kijamii) kuiwezesha kuhukumiwa kwa Tuzo na Baraza la Waamuzi au kura ya umma.

(5) Ni kuhusiana na picha yoyote unayowasilisha ambayo inashinda Tuzo, inayozingatiwa kushinda Tuzo na isiyohitaji kulipiwa nyongeza yoyote isipokuwa kama imeelezwa vinginevyo, ndio unatuidhinisha sisi, Jumba la Makumbusho, na ikiwa lazima mashirikamawakala wowote wanaotenda kwa niaba yetu, haki wakati wa Kipindi cha Leseni:

(i) kutoa upya na kuonyesha picha katika Maonyesho yoyote kwa chapa au kidijitali:

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.

# Wildlife Photographer of the Year

(ii) kutumia picha hiyo katika muundo wowote (iliyofafanuliwa katika kifungu cha 8 (12)) kutangaza na kukuza Mashindano yoyote au Maonyesho, bila malipo zaidi kasoro kama imeelezwa katika kifungu cha 8 (5) (v) hapa chini;

(iii) kutoa kibali tegemezi kwa Wa/Mdhamini Rasmi kutumia picha hiyo ili kutangaza na kusherehekea Shindano au Maonyesho ya WPY na uhusiano wao nao kwa njia yoyote (iliyofafanuliwa katika kifungu cha 8 (12));

(iv) kutoa kibali tegemezi kwa Ziara ya Maonyesho au mwendeshaji ("Mmiliki Leseni ya Ziaraya Maonyesho") kuchapisha au kuandaa uchapishaji wa picha yako kwa maonyesho katika ukumbi wao wa Ziara ya Maonyesho, onyesha picha yako katika ukumbi wa Ziara ya Maonyesho kwa chapa au kwa kidijitali na kutangaza na kukuza Ziara yao ya Maonyesho kwa njia yoyote (iliyofafanuliwa katika kifungu cha 8 (12)) huku mtoa leseni wa Ziara ya Maonesho akiwa na haki kutoa leseni zaidi kwa Mfadhili wao wa Ziara ya Maonesho (ikiwa ameidhinishwa na NHM) kutumia picha kutangaza na kusherehekea Ziara ya Maonesho na uhusiano wa Mfadhili wa Ziara ya Maonesho kutumia njia yoyote (ilivyoelezewa kwenye sehemu ya 8(12)) wakati wa kipindi cha Ziara hiyo ya Maonesho; na/au

(v) chapisha picha yako au mfano wako katika Kitabu cha Jalada cha kila mwaka au Kitabu cha Viangazio. Uamuzi wowote wa kutumia haki hiyo utakuwa kwa hiari ya Jumba la Makumbusho lakini ikiwa itatumika basi, Jumba la Makumbusho litakulipa ada ifuatayo: ukurasa wa mbele wa jalada £250.00; ukurasa wa nyuma wa jalada £150.00; matoleo ya ushirikiano ukurasa wa mbele wa jaladakama haujatumika bado kwenye toleo la Uingereza £120.00; matoleo ya ushirikiano ukurasa wa mbele wa jaladakama haujatumika bado kwenyetoleo la Uingereza £75.00; Viangazio ukurasa wa mbele wajalada £150.00; picha moja moja £75.00 (zinaweza kutumika katika Jalada na Viangazio kwa ada moja); Jalada, 'Nyota ya Kesho' na simulizi za Uandishi wa Habari kwa kutumia picha £375.00 kwa mkusanyiko.

(6) Fursa zingine za kibiashara zinaweza kupatikana kwako ili ufaidike kutokana na matumizi ya wasilisho lolote lilichochaguliwa na Baraza la Waamuzi. Pale mbapo faida kama hiyo ya kibiashara inaweza kutokea, tutatafuta idhini yako mapema na kukupa leseni inayofaa. Mifano ni pamoja na:

(i) kujumuishwa katika uongezaji soko kwa kutumia alama bainifu unaohusishwa na Shindano, au Maonyesho yoyote, kasoro ya Kitabu cha Jalada na kitabu cha Viangazio; na

(ii) kutoaleseni ya uongezaji soko kwa kutumia alama bainifu kwa mtu mwingine.

(7) Kipindi cha Leseni:

(i) kitaanza tarehe utakapoarifiwa juu ya Tuzo lako na kuendelea kwa kipindi cha miaka mitano (5); na

(ii) baada ya kipindi tajwa

a. Jumba la Makumbusho litahifadhi nakala za picha (elektroniki au vinginevyo) na

b. Jumba la Makumbusho na Mwenye Leseni ya Ziara ya Maonesho watahifadhi nakala za (kielektroniki au vinginevyo) za nyenzo za matangazo au kibiashara zilizotengenezwa kuchapisha, kutangaza au kufanyia Shindano au Onesho biashara lakini katika kesi zote mbili ni lazima zitatafuta idhini yako ikiwa tunataka au wanatumai kutumia picha hizo kwa madhumuni zaidi.

(8) Sisi, Jumba la Makumbusho na mashirika yoyote yaliyo na leseni chini ya kifungu cha 8 (5) tutakupa sifa, au (kama tofauti) mpiga picha, wakati tunatumia picha kulingana na Masharti haya. Pamoja na hayo, unakubali, kwamba hatutawajibika kwako, au (kama tofauti) mpiga picha, ikitokea bila kukusudia kukosa kuonyesha sifa hiyo.

(9) Ni lazima uhakikishe kwamba:

(i) picha zozote unazowasilisha zimepigwa kwa idhini ya:

a. mtu yeyote anayetambulika katika picha hiyo; au

b. idhini ya mzazi / mlezi wake ikiwa kama yuko chini ya miaka 16, na

(ii) kwamba watu hao wameshauriwa:

a. kwamba picha inaweza kuwasilishwa kwenyeShindano; na

b. kwamba picha yake inaweza ikatumika kufuatana na Masharti haya.

(10) Unakubali kwamba uwasilisho kwenye Shindano hautoi haki zozote kuhusiana na majina, nembo au mali ya akili yoyote inayohusiana au inayomilikiwa nasi, Jumba la Makumbusho au Shindano. Unakubali kutotoa tamko lolote hadharani kwa kutumia majina, nembo au mali za akili hizozozote bila idhini yetu ya kimaandishi ya awali.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.

# Wildlife Photographer of the Year

(11) Tutakumbusha umma kuwa hakimiliki ya picha za Maonyesho zinabaki kwa wapiga picha na hatutahimiza umma moja kwa moja kuchapisha picha za Maonyesho kwenye akaunti zao za kibinafsi za mitandao ya kijamii. Hata hivyo, unatambua kwamba sisi wala Makumbusho, wala Wamiliki wa Leseni za Ziara ya Maonyesho tuna uwezo wa kikweli kweli wa kuzuia hali hii kutokea. Una samehe haki yoyote ambayo unaweza kuwa nayo (kama ipo) ya kuleta madai dhidi yetu, Jumba la Makumbusho au Wamiliki wa Leseni za Ziara ya Maonyesho ikiwa kama matokeo ya kushindwa kuzuia umma kupiga au kushiriki picha za Maonyesho.

(12) Histilahi ya "njia yoyote" inapotumika katika kifungu cha 8 (5) itajumuisha lakini sio tu chapa, kitabu, jarida, wadau wa mawasiliano wa NHM, (media za kidijitali, programu au idhaa za mitandao ya kijamii) wowote.

(13) Tuna haki bila ya kukujulisha kabla kubatilisha ingizo, au kuondoa picha kutoka kwenye Shindano au Onesho, ikiwa kwa busara yetu pekee lakini kwa kutenda kwa mashiko tukikuta onesho letu linakuwa la kihalifu au linakiuka haki za mshirika.

## 9. ZUIO LA UWAJIBIKAJI

(1) Uthibitisho wa uwasilishaji wa kielektroniki sio ushahidi wa kupokelewa nasi.

(2) Hatuwezi kuwajibika kwaajili ya barua pepe ambazo hazifiki kwa sababu ya mipangilio yako ya usalama wa barua pepe au vizuizi vilivyowekwa na Mtoa Huduma wako wa Mtandao. Lazima uhakikishe kuwa mipangilio yako inakubali barua pepe kutoka kwa **wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk** na **msonlineservicesteam@microsoftonline.com**.

(3) Wasilisho za kidijitali kwenye Shindano hazitahifadhiwa au kurudishwa na sisi baada ya majina ya wapiga picha waliopewa tuzo kutangazwa

(4) Kasoro pale ilipoelezewa dhairi sehemu nyingine katika Mashartina kwa kiwango kamili kinachoruhusiwa na sheria, hatutawajibika kwa hasara au uharibifu wowote utakaokabiliana nao kuhusiana na Shindano, matumizi ya uwasilisho lako kulingana na Mashartihaya au matumizi ya zawadi yoyote. Kinga hii ya dhimaitajumuisha lakini sio tu dhima dhidi ya hasara yoyote au uharibifu kwauwasilisho wowote, dhima dhidi ya utumiaji mbaya wa picha; na/au kushindwa kwa mmiliki mwingine yeyote wa leseni kutii majukumu ya mikopo katika Masharti haya.

## 10. ULINZI WA DATA

Tutakusanya data zako za kibinafsi (na za mzazi/ lezi wako pale inapofaa) wakati wa usajili, na kama ilivyoonyeshwa vinginevyo ili kusimamia Shindano, Maonyesho na/au shughuli husussan. Kwa taarifa zaidi juu ya jinsi sisi na Jumba la Makumbusho tunavyochakata data za kibinafsi tafadhali angalia Ilani yetu ya Faragha hapa **https://www.nhm.ac.uk/about-us/privacy-notice.html**.

## 11. MATUKIO NJE YA UWEZO WA KAWAIDA WA MMILIKI

Hatukuwa tumekiuka Masharti haya wala hatutawajibika kwa kuchelewesha kutekeleza, au kutotimiza majukumu yake yoyote chini ya Masharti haya ikiwa kuchelewa huko au kutotimiza kunatokana na matukio, hali au sababu zilizo nje ya uwezo wetu wa kawaida. Katika hali kama hizo, tutakuwa na haki ya kuwa na muda wa nyongeza wa kiasi kilicho cha sawakwa ajili ya kutekeleza majukumu kama hayo. Ikiwa kipindi cha kuchelewa au kutofanya kazi kinaendelea kwa wiki 1, tunaweza kusitisha mkataba na wewe ulioundwa na Masharti haya kwa kukupa ilani ya siku 14 kwa maandishi.

## 12. MKATABA WOTE

Masharti haya na tovuti au hati nyingine zilizojumuishwa vinafanya sehemu kamili ya mkataba kati yako na sisi na huchukua nafasi na kubatilisha mikataba ya awali, ahadi, dhima, dhamana, uwakilishi na uelewa kati yao, iwe vya maandishi au mdomo, inayohusiana na mada yake, ikiwemo lakini sio nyaraka za matangazo au ukuzaji. Unakubali kuwa hautakuwa na suluhu kuhusu tamko, uwakilishi, ahadi au dhamana yoyote (iwe imetolewa kwa kutojua au kwa uzembe) ambayo haijawekwa katika Masharti haya.

## 13. HAKI ZA MTU ALIYE NNJE YA MAPATANO HAYA

Zaidi ya haki zilizotajwa dhairi zinazohusu sisi, Jumba la Makumbusho, Wa/Mfadhili Rasmi, Mfadhili (Wafadhili) wa Ziara ya Onesho, au Wa/Mmiliki Leseni za Ziara ya Maonyesh, mkataba na leseni iliyokuwepo kutokana na uwasilishaji kufuatana na Masharti haya havitoi haki kwa mtu mwingine chini ya Sheria ya Mikataba (Haki za Mtu Wengine) ya 1999 [Contracts (Rights of Third Parties) Act 1999] ili kutekelezesha vifungu vyovyote vya Masharti haya.

## 14. SHERIA NA MAMLAKA

Mashartiyatasimamiwana kutafsiriwa kwa mujibu wa sheria za Uingereza na Wales na wahusika watawajibika chini ya mamlaka peke ya mahakama za Uingereza na Wales.

E-mail:
wildlifephotographeroftheyear@nhm.ac.uk
Website:
**wildlifephotographeroftheyear.com**

Natural History Museum

© The Trustees of the Natural History Museum, London.